JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM



# TAARIFA YA MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA MAENDELEO YA TAIFA KWA MWAKA 2021

Septemba, 2022

**YALIYOMO**

YALIYOMO ..... i
VIFUPISHO ..... iii
ORODHA YA MAJEDWALI ..... iv
ORODHA YA MAUMBO ..... v
DIBAJI ..... vi
SHUKRANI ..... vii
TAARIFA KWA UFUPI ..... viii
SURA YA KWANZA ..... 1
UTANGULIZI ..... 1
1.1 Mamlaka ya Uratibu ..... 1
1.2 Msingi wa Taarifa ..... 2
1.3 Malengo ya Taarifa ..... 2
1.4 Walengwa wa Taarifa ..... 3
1.5 Mawanda ya Uchambuzi ..... 3
1.6 Mbinu za Utafiti ..... 3
SURA YA PILI ..... 4
MFUMO WA KISHERIA WA URATIBU WA MASHIRIKA ..... 4
2.1 Mfumo wa Kisheria ..... 4
2.2 Mwongozo wa Uratibu ..... 4
2.3 Mfumo wa Kielektroniki ..... 4
2.4 Mahitaji ya Kisheria ..... 4
2.5. Uwasilishaji wa Taarifa ..... 5
SURA YA TATU ..... 6
MAPATO, MATUMIZI NA UENDELEVU WA MASHIRIKA ..... 6
3.1 Mapato ya Mashirika ..... 6
3.2 Matumizi ya Mashirika ..... 7
3.3 Uendelevu wa Mashirika ..... 8
SURA YA NNE ..... 9
MCHANGO WA MASHIRIKA KWA MAENDELEO YA NCHI ..... 9

4.1 Utekelezaji wa Miradi ........ 9

4.2 Utekelezaji wa Miradi Kisekta ........ 10

4.2.1 Sekta ya Afya ........ 10

4.2.2 Uwezeshaji wa Jamii ........ 10

4.2.3 Ulinzi wa Jamii ........ 11

4.2.4 Uhifadhi wa Mazingira ........ 12

4.2.5 Sekta ya Kilimo ........ 12

4.2.6 Sekta ya Elimu ........ 12

4.2.7 Utawala Bora ........ 13

4.2.8 Sekta ya Maji ........ 13

4.2.9 Haki za Binadamu ........ 14

4.2.10 Usawa wa Kijinsia ........ 14

4.2.11 Sekta ya Nishati ........ 15

4.3 Wanufaika wa Miradi ........ 15

4.4 Ajira za Mashirika ........ 17

4.5 Michango ya Hifadhi ya Jamii ........ 18

SURA YA TANO ........ 19

HITIMISHO ........ 19

5.1 Utangulizi ........ 19

5.2 Changamoto ........ 19

5.3 Mapendekezo ........ 19

REJEA ........ 21

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGRA | Alliance for Green Revolution in Africa |
| BMZ | Germany Federal Ministry for Economic Coopration and Development |
| CCBRT | Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania |
| CDC | Centre for Disease and Control |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DDA | Data Driven Advocacy |
| DFID | Department for International Development |
| E.U | European Union |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| HPSS | Health Promotion and System Strengthening |
| JMT | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| GIZ | Germany Agency for International Cooperation |
| G.N | Government Notice |
| KOICA | Korean International Cooperation Agency |
| MDH | Management and Development for Health |
| MSPH | Mailman School of Public Health |
| NaCoNGO | National Council for Non-Governmental Organizations |
| NGOs | Non-Governmental Organizations |
| NIDA | National Identification Authority |
| NIS | NGOs Information System |
| NORAD | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| SIDA | Swedish International Development Cooperation Agency |
| UNICEF | United Nations Children Fund |
| UNHCR | United Nations High Commision for Refugees |
| USAID | United States Agency for International Development |
| VST | Village School Tanzania |
| WWF | World Wildlife Fund |

## ORODHA YA MAJEDWALI


| | |
|---|---|
| JEDWALI 3.1 | Vyanzo vya Fedha vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| JEDWALI 4.1 | Mchanganuo wa Fedha za Miradi kwa Kila Sekta/Afua kwa Mwaka 2021 |
| JEDWALI 4.3 | Wanufaika wa Miradi kwa Kila Sekta/Afua |
| JEDWALI 4.4 | Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa kwa Watanzania na Wageni |

**ORODHA YA MAUMBO**


Umbo 1.1 Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali
Umbo 3.1 Vyanzo vya Fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali
Umbo 3.2 Matumizi ya Fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali
Umbo 4.1 Asilimia ya Fedha Iliyotumika kwa Kila Sekta/Afua
Umbo 4.3 Asilimia ya Wanufaika kwa Makundi
Umbo 4.4 Asilimia ya Waajiriwa na Wanaojitolea kwa Watanzania na Wageni

# DIBAJI

Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 inaweka msingi wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Pamoja na mambo mengine, Sera hii ilitoa maana ya Shirika Lisilo la Kiserikali, kuainisha vyombo vya usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuweka utaratibu wa kusajili Mashirika. Sera hii ilipelekea kutungwa kwa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania Bara ambayo imempa mamlaka Msajili kusajili na kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara.

Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kukua kuanzia mwaka 2005 ambapo kulikuwa na Mashirika 2110 hadi Mashirika 6120 kufikia Disemba 2021, na hivyo ni muhimu mchango wa Sekta hiyo kutambuliwa na Serikali. Ni matarajio ya Serikali kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatafanya kazi kwa kwa Kuzingatia Sheria na Miongozo hasa katika kuihudumia jamii kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji.

Hivyo, katika kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imeandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2021. Taarifa hii pamoja na mambo mengine imeainisha taratibu za kisheria za uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, pia inaonesha mchango wa Mashirika katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la afya, uwezeshaji wa jamii, ulinzi wa jamii, mazingira, kilimo, Elimu, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia. Aidha, imeainisha changamoto na namna ya kutatua changamoto zilizopo.

Katika kuhakikisha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaendelea kutoa mchango wake katika maendeleo ya Taifa, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kutambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya kiserikali katika nyanja za kijamii na kiuchumi kupitia miradi inayotekelezwa katika sekta/afua mbalimbali nchini. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali inahimiza misingi ya uwazi, uwajibikaji na ushirikiano katika utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kufanya shughuli za maendeleo.

Aidha, ni matumaini yetu kuwa taarifa hii itakuwa ni chachu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine kuendelea kuboresha huduma kwa jamii. Vilevile, taarifa hii itaongeza ufanisi na tija katika kuratibu na kusimamia shughuli za Masharika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha kuwa mchango wake unaendelea kutambulika kwa kuimarisha mifumo ya kiutendaji na ushirikiano baina ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Dkt. Zainab A.S. Chaula

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**SHUKRANI**


Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inapenda kutoa shukrani za pekee kwa watu wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuandaa taarifa na na kuchapisha kitabu hiki cha mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa maendeleo ya Taifa.

Shukrani za dhati ziende kwa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya aliyekuwa Mwenyekiti, Dkt. Richard Sambaiga, pamoja na Mwenyekiti wa sasa, Bi. Mwantumu Mahiza kwa uongozi na maelekezo katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara na uandaaji wa taarifa hii.. Aidha, shukrani zilifikie Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Lilian Badi kwa kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha zilizosaidia kukamilisha uandaaji wa taarifa hii.

Vilevile, shukrani ziende kwa uongozi wa Wizara kwa kutoa mchango wao wa hali na mali katika utoaji wa mawazo na maelekezo mbalimbali katika kukamilisha shughuli za uandaaji wa kitabu cha mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

Hali kadhalika, shukrani ziifikie timu ya wataalamu ambayo imeshiriki kuandaa taarifa hii na na kuisambaza kwa wadau mbalimbali.Timu hii iliongozwa na Charles Komba (Mwenyekiti), Musa Leitura, Faki Shaweji (Katibu), Jaina Saidi Msangi, Francisca Ng'wendesha, Charles Mpaka, Wende Saga, Lilian Mganda na Issa Mtinangi.

Kipekee shukrani ziyaendee Mashirika ya Pact Tanzania na Freedom House kupitia mradi wa DDA, Rikolto, HPSS na Taasisi ya Speedy Print Ltd zilizofanikisha uandaaji wa Kitabu hiki kwa kutoa mchango wa fedha zilizofanikisha uandaaji wa Kitabu hiki.



Vickness G. Mayao

**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

**TAARIFA KWA UFUPI**

Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni kati ya wadau muhimu wa kimkakati katika kukuza maendeleo ya jamii ndani na nje ya Tanzania. Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi maalum ina jukumu la kusimamia uratibu wa sekta hii kwa mujibu wa Sera, Sheria na Miongozo ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

Taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni nyenzo muhimu ya kupima utendaji kazi wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika.Taarifa hii imegawanyika katika Sura kuu Tano. Sura ya kwanza, inaoneshautangulizi unaojumuisha mamlaka ya uratibu, msingi wa uchambuzi, malengo, mawanda na njia za utafiti. Sura ya pili, ni mfumo wa kisheria wa uratibu wa Mashirika inayojumuisha maelezo ya Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika, mahitaji ya kisheria na uwasilishaji wa taarifa.

Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa umeelezewa katikasura ya tatu na nne ambapo taarifa za Mashirika 955 zimechambuliwa zikiwa na jumla ya mapato ya shilingi **1,194,306,453,232** na matumizi ya shilingi **1,081,499,948,916**. Uchambuzi unaonesha kuwa, Mashirika mengi yanazingatia viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha na uendeshaji wa Mashirika, ingawa Mashirika mengi yanategemea zaidi chanzo kimoja cha mapato (ufadhili kutoka nje) jambo ambalo linaweza kusababisha mashirika hayo kukosa uendelevu endapo itatokea vipaumbele vya wafadhili kubadilika.

Uchambuzi huu unaonesha kuwa Mashirika yametoa mchango mkubwa katika sekta/afua za Afya, Uwezeshaji wa jamii, Ulinzi wa Jamii, Mazingira, Kilimo, Elimu, Utawala Bora, Maji, Haki za Binadamu na Jinsia. Aidha, kazi na huduma za Mashirika hayo ziliwanufaisha watu **79,216,986** kati yao wanawake **24,387,249**, wanaume **8,696,126, watoto 4,004, 510, Wazee 3,495,055,** Vijana **38,587,098**, wajane 25, 417 na watu wenye ulemavu **18,53**1. Aidha, jumla ya Taasisi **2,350,823** zilinufaika kutokana na huduma za Mashirika. Kwa upande wa ajira, Mashirika yameajiri jumla ya watu **14,121** ambao wengi ni watanzania.

Sura ya tano ni hitimisho na mapendekezo ambapo inaelezea umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika uzalishaji wa ajira na kuchangia maendeleo ya jamii kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa. Aidha, ilionesha kuwa changamoto kubwa ni uwasilishaji usioridhisha wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na uelewa mdogo wa matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hivyo, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhakikisha taarifa zao zinawasilishwa kupitia mfumo na mchango wao kutambulika.

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Mamlaka ya Uratibu


Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kusajili na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.3 ya Mwaka 2019.

Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeelekeza kuhusu suala la uwazi na uwajibikaji kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na ubia kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambapo inatambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika jamii. Katika kutekeleza hilo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakiwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi wanazofanya katika kipindi cha robo mwaka na mwaka ili kuwezesha kujua shughuli zilizotekelezwa pamoja na mchango wake katika maendeleo ya Taifa.

Wizara pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikifanya ufuatiliaji wa shughuli/miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lengo ni kutathmini mchango unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya nchi, tija ya miradi inayotekelezwa kwa jamii kulingana na Sera za Nchi na kupima mwenendo wa utekelezaji wa majukumu ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia sekta hii ikiwa ni pamoja na kufahamu mafanikio na changamoto za kiutendaji katika sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

Kwa mwaka 2021, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake katika maeneo ya usajili, uratibu, ufuatiliaji na uchambuzi wa mikataba ya ufadhili. Katika kipindi cha Januari – Desemba 2021 jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **1,164** yamesajiliwa kati ya Mashirika hayo **65** ni ya Kimataifa **1099 ni ya** Kitaifa na kufikia jumla ya Mashirika yote yaliyo hai **6,901** hadi Desemba 2021**.**

**Umbo 1.1 Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**




Aidha, Wizara ilifanya zoezi la uhakiki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kupata idadi sahihi ya Mashirika yaliyo hai na yanayotekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania Bara na kuhuisha kanzidata ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 4,864 yalihakikiwa na kutangazwa kwenye tovuti ya Wizara (www.jamii.go.tz) hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2022. Kufuatia zoezi hilo, Jumla ya Mashirika 4,909 yalisimamishiwa usajili na kupelekea kanzidata ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na Mashirika **6,120** yaliyo hai kati ya Mashirika **12,442** yaliyokuwa yamesajiliwa hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2022 sawa na asilimia 49.

Vilevile, katika kipindi cha mwaka 2021 Mashirika **55** yamewasilisha Mikataba/Makubaliano ya fedha za ufadhili wa miradi kwa mujibu wa Marekebisho ya Kanuni, Tangazo la Serikali Na. 609/2018. Jumla ya mikataba/makubaliano **115** yenye kiasi cha shilingi **77,963,519,594** yalimewasilishwa, kufanyiwa uchambuzi na kuidhinishiwa ili yaweze kutekeleza miradi.

## 1.2 Msingi wa Taarifa

Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na uhitaji wa taarifa sahihi za mchango wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wadau wa Maendeleo, Taasisi za Utafiti, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Serikali imekuwa ikihitaji taarifa sahihi kuhusu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kutambua mchango wake katika pato la taifa na kuwataarifu watunga Sera na wafanya maamuzi. Hivyo, tathmini ya mwaka 2021 ya Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inatoa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kitakwimu kwa ajili ya Maendeleo ya Taifa na kutambua fursa mbalimbali ili kuboresha sekta.

## 1.3 Malengo ya Taarifa

Lengo kuu la kuandaa taarifa hii ni kutathmini na kupata picha halisi ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa kupitia utekelezaji wa kazi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwa kipindi cha mwaka 2021.
Malengo Mahsusi ni pamoja na;

a) Kutambua idadi ya Mashirika yaliyosajiliwa kwa mwaka 2021;

b) Kutambua idadi ya Mashirika yaliyowasilisha mikataba ya fedha;

c) Kutambua Mashirika yaliyowasilisha taarifa ya utendaji ya mwaka na kuainisha miradi inayotekelezwa pamoja na matumizi ya rasilimali; na

d) Kutambua changamoto na jinsi ya kuzitatua.

### 1.4 Walengwa wa Taarifa

Taarifa hii inalengwa kutumiwa na Wizara yenye dhamana na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

### 1.5 Mawanda ya Uchambuzi

Uchambuzi huu unaonesha mchango wa Mashirika Yasiyo ya kiserikali katika nyanja za kiuchumi na kijamii, uzingatiaji wa Sheria na Miongozo, uzingatiaji wa mipango ya kitaifa, upatikanaji wa fedha na uendelevu wa sekta. Uchambuzi huu unahusisha jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **955** miongoni mwa hayo Mashirika **213** ya kimataifa na **742** ya kitaifa kati ya **6,120** yaliyopaswa kuwasilisha taarifa za mwaka 2021.

### 1.6 Mbinu za Utafiti

Kimsingi, taarifa hii imeandaliwa kwa kuchambua ripoti mbalimbali za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zilizowasilishwa kwa mwaka 2021 zikiwemo taarifa za mwaka, mikataba ya fedha kwa kuangalia afua zilizotekelezwa, mapato na matumizi, ajira na wanufaika wa miradi iliyotekelezwa.

## SURA YA PILI
## MFUMO WA KISHERIA WA URATIBU WA MASHIRIKA

### 2.1 Mfumo wa Kisheria

Tanzania Bara, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaongozwa kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001) na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Kwa kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana hadhi ya kisheria (legal personality) yanaweza kuingia mikataba, kushtaki au kushtakiwa kwa jina la Shirika kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 18 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 31 (a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali , Sura ya 56, Mashirika yanapaswa kuzingatia Sheria mbalimbali kwenye utekelezaji wa majukumu yao mathalani Sheria za Uhamiaji, Kodi, Ajira pamoja na kuheshimu mila na desturi za watu na jamii wanapotekeleza shughuli zao.

### 2.2 Mwongozo wa Uratibu

Katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara iliandaa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wa mwaka 2020 ambao umeainisha majukumu na wajibu wa kila mdau wa Sekta katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara. Mwongozo huu una lengo la kuondoa mgongano wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kurahisisha uratibu wa pamoja.

### 2.3 Mfumo wa Kielektroniki

Katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kieletroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (nis.jamii.go.tz) ambao umeanza kutumika rasmi Mei, 2020. Aidha, Mfumo huo umewezesha usajili wa Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali, upokeaji wa taarifa za robo na mwaka za Mashirika, uhuishaji wa taarifa mbalimbali za shirika, upokeaji wa mikataba ya fedha na ulipaji wa ada za mwaka. Aidha, mfumo huo umeunganishwa na mifumo mingine kama vile Mfumo wa vitambulisho vya utaifa (NIDA) na mfumo wa kielekroniki wa malipo ya Serikali (GePG).

### 2.4 Mahitaji ya Kisheria

Kwa ujumla, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

a) Kuwasilisha taarifa za robo mwaka kwa mujibu wa kanuni ya 20 ya marekebisho ya kanuni za mwaka 2019 ( Tangazo la Serikali Na. 685/2019);

b) Kuwasilisha taarifa za mwaka na taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 29 (1) (a) na (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania Bara;

c) Kufanya uhuishaji wa Taarifa za Mashirika, kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania Bara;

d) Kulipa ada ya mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 38 (2) (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania Bara;

e) Kutoa taarifa za wanufaika wa miradi kwa mujibu wa Kanuni ya 13 (a) ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Tangazo la Serikali, 608/2018;

f) Kutangaza vyanzo vya mapato mara mbili kwa kila mwaka, uwasilishaji wa mikataba ya fedha na kutoa taarifa ya fedha inayozidi kiasi cha shilingi milioni ishirini (Shilingi 20,000,000) kwa mujibu wa kanuni ya 13 (a) (b) na (c) ya marekebisho ya kanuni ya mwaka 2018 (Tangazo la Serikali Na. 609/2018).

## 2.5. Uwasilishaji wa Taarifa

Taairifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya ya Kiserikali ni ya tatu kuandaliwa na Wizara (2015, 2020 na 2021). Katika kipindi cha mwaka 2021, Mashirika **955** yamewasilisha taarifa za utekelezaji kati ya Mashirika **5,595** yaliyopaswa kuwasilisha taarifa ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ya Mashirika yaliyowasilisha taarifa za utekelezaji kwa 2020. Aidha, jumla ya Mashirika **2,441** yamelipa ada za mwaka sawa na asilimia 40 ya Mashirika yaliyopaswa kulipa ada. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, Mashirika mengi yanalipa ada bila kuwasilisha taarifa za utekelezaji hivyo kusababisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mashirika kushindwa kuonesha kwa ukamilifu mchango wa Mashirika katika maendeleo ya Taifa.

## SURA YA TATU
## MAPATO, MATUMIZI NA UENDELEVU WA MASHIRIKA


### 3.1 Mapato ya Mashirika

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2021 taarifa inaonesha kuwa, mashirika **955** yaliyowasilisha taarifa yalipata fedha kiasi cha shilingi **1,194,306,453,232** kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwa ni upungufu wa asilimia 17 wa mapato ya Mashirika kwa mwaka 2020. Kiasi hiko cha mapato ya fedha za Mashirika ni asilimia 3 ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022. Mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka husika yameainishwa hapo chini.

**JEDWALI 3.1: Vyanzo vya Fedha**

| NA. | CHANZO | KIASI |
|---|---|---|
| **1** | Bakaa | 20,737,107,780 |
| **2** | Msamaha wa kodi | 257,949,320 |
| **3** | Ruzuku | 40,600,000 |
| **4** | Michango ya wanachama | 8,629,129,324 |
| **5** | Mapato ya vitega uchumi | 5,282,542,650 |
| **6** | Malipo ya Huduma | 817,156,221 |
| **7** | Michango ya jamii | 12,273,273,853 |
| **8** | Wafadhili wa ndani | 11,882,369,268 |
| **9** | Michango kutoka Sekta Binafsi | 2,036,647,563 |
| **10** | Wafadhili wa nje | 1,132,349,677,253 |
| | **Jumla** | **1,194,306,453,232** |

**Umbo 3.1 Vyanzo vya Fedha**





Taarifa hii ya mapato inaonesha kuwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Kwa asilimia kubwa yanategemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje. Hata hivyo, inaonesha kuwa mfumo wa kisheria wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unaoruhusu Mashirika kuwekeza katika miradi ya uzalishaji unafanya kuwa ni chanzo muhimu cha kujipatia kipato kwa uendelevu wa Mashirika hayo.

Aidha, mchango wa jamii katika kutekeleza miradi ya mashirika inaonekana kukua hali ambayo inaashiria uwepo wa ubia kati ya mashirika na jamii. Hata hivyo, nguvu zaidi inatakiwa kuwekezwa katika kuyawezesha na kuhimiza mashirika kwenye eneo la kuwekeza kwenye miradi ya kujipatia kipato na uingiaji wa ubia kati ya Mashirika na jamii ili vyanzo hivyo viendelee kukua.

### 3.2 Matumizi ya Mashirika

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2021 taarifa zinaonesha kuwa, kiasi cha shilingi **1,081,499,948,916** kimetumika kama ilivyoainishwa hapo chini:-

**Umbo 3.2 Matumizi ya Fedha**



| | Miradi | Posho na Mishahara | Kodi inayotokana na Ujuzi | Kodi Makato ya Mishahara | Mfuko wa Taifa wa hifadhi ya Jamii | Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kiasi cha fedha | 942,794,477,792 | 109,686,581,004 | 1,774,979,633 | 13,813,995,233 | 12,700,469,371 | 729,445,883 |
| asilimia | 87.17% | 10.14% | 0.16% | 1.28% | 1.17% | 0.07% |

Taarifa hii ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2021 inaonesha kuwa kiasi kikubwa kimetumika katika utekelezaji wa miradi, kulipia kodi za Serikali na ulipaji wa mishahara kwa wafanyakazi.

### 3.3 Uendelevu wa Mashirika

Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 inayapa Mashirika uwezo wa kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na michango ya wanachama, ufadhili, miradi ya maendeleo, misamaha ya kodi na ruzuku kutoka Serikalini.

Aidha, uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa Mashirika mengi yamekuwa yakitegemea zaidi ufadhili hali ambayo inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi katika jamii. Kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa agizo la kuandaa mkakati wa Kitaifa wa uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kutatua changamoto za upatikanaji wa fedha.

Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama hatua ya kupunguza utegemezi na kuyawezesha Mashirika hayo kuwa himilivu.

# SURA YA NNE
# MCHANGO WA MASHIRIKA KWA MAENDELEO YA NCHI

## 4.1 Utekelezaji wa Miradi

Mwaka 2001, Serikali ilitunga Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika kujiendesha vizuri na kwa ufanisi katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Sera hiyo imeweka misingi thabiti ya kutambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya nchi kama wadau muhimu na kuweka mifumo ya utekelezaji wake kupitia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 na Kanuni zake.


Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuzingatia Sera, Sheria na Mipango ya Kitaifa inayosimamia Sekta/afua za utekelezaji ikiwa ni pamoja na Sera ya Afya (2007), Sera ya Uhifadhi wa Jamii (2003), Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Kilimo (2013), Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Sera ya Taifa ya Mazingira (1997), Sera ya Taifa ya Maji (2002), Sera ya Maendeleo ya Jinsia (2002), Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013) pamoja na nyingine.

Kwa kipindi cha mwaka 2021, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametumia kiasi cha shilingi **942,794,477,792** kutekeleza jumla ya Miradi 1,987 katika Sekta/Afua za Afya, Uwezeshaji wa jamii, Ulinzi wa Jamii, Mazingira, Kilimo, Elimu, Utawala Bora, Maji, Haki za Binadamu Jinsia na Nishati.

**Jedwali 4.1: Mchanganuo wa Fedha Kisekta**

| Na. | Sekta/Afua | Kiasi cha fedha |
|---|---|---|
| 1. | Afya | 360,810,724,455 |
| 2. | Uwezeshaji wa jamii | 332,239,023,518 |
| 3. | Ulinzi wa jamii | 61,478,824,070 |
| 4. | Mazingira | 52,324,452,813 |
| 5. | Kilimo | 47,306,774,582 |
| 6. | Elimu | 44,000,586,605 |
| 7. | Utawala Bora | 18,426,362,089 |
| 8. | Maji | 10,449,181,801 |
| 9. | Haki za binadamu | 9,799,297,602 |
| 10. | Jinsia | 4,517,067,410 |
| 11. | Nishati | 1,442,182,847 |
| | **Jumla** | **942,794,477,792** |

**Umbo 4.1: Asilimia ya Fedha Kisekta**




## 4.2 Utekelezaji wa Miradi Kisekta

### 4.2.1 Sekta ya Afya

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa kwenye sekta ya afya ambapo baadhi yanaendesha hospitali, vituo vya afya, zahanati na vituo vya mafunzo ya afya. Aidha, Mashirika mengine yanaendelea kufadhili huduma za afya kama vile UKIMWI, kifua kikuu, malaria, tohara, lishe, afya ya mama na mtoto na UVIKO 19.

Kwa mwaka 2021, sekta ya afya imeongoza kwa kuwa na fedha nyingi ambayo ni Shilingi **360,810,724,455** sawa na asilimia **38.3** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimetekelezwa katika masuala ya UKIMWI, malaria, lishe na afya ya uzazi.

Uchambuzi unaonesha kuwa wafadhili wakubwa wa sekta ya Afya ni USAID, UNICEF, Bill and Melinda Gate, GLOBAL FUND na CDC.

### 4.2.2 Uwezeshaji wa Jamii

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni moja ya wadau muhimu katika kuiwezesha jamii hususani katika kuunga mkono jitihada za jamii na kuimarisha uwezo wao wa kujitegemea.

Kwa mwaka 2021, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliwezesha vikundi mbalimbali vikiwemo vya wanawake na vijana kwenye nyanja za ujasiriamali, huduma za uwekaji

na ukopaji wa fedha, mafunzo ya ufundi, uzalishaji na uongezaji thamani wa bidhaa pamoja na mafunzo ya uongozi.

Aidha, Sekta ya uwezeshaji wa jamii imeongoza kwa kuwa na miradi mingi ya utekelezaji na ya pili kwa kiwango cha fedha ambapo kiasi cha Shilingi 332,239,023,518 kimetumika sawa na asilimia **35.2** ya fedha zote zilizotekeleza miradi.

Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekelezwa katika kuiwezesha jamii katika masuala ya kuongeza ujuzi wa uzalishaji kwa wazalishaji mali wadogo, kujenga uwezo wa wajasiriamali wadogo na wakati, kujenga uwezo wa asasi za kiraia, kujenga uwezo kwa vijana na wanawake.

Uchambuzi unaonesha kuwa, katika sekta ya Uwezeshaji wa jamii, wafadhili wakubwa ni Bill and Melinda Gates Foundation, Fintrac HQ, Innovation for Poverty Action, MasterCard Foundation na Policy Forum.

### 4.2.3 Ulinzi wa Jamii

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa kwenye jitihada za pamoja katika kuanzisha na kuhamasisha jamii kupitia programu mbalimbali za ulinzi wa jamii hususan za kulinda maslahi na ustawi wa watoto, wazee, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, yatima na makundi maalum.

Ulinzi wa jamii ulihusisha utekelezaji wa miradi ya uendeshaji wa makao ya watoto, nyumba salama, makazi ya wazee, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya ulinzi wa jamii imetumia kiasi cha Shilingi **61,478,824,070** sawa na asilimia **7** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya kusaidia makundi maalum kama vile watoto yatima, wazee, wajane na vijana pamoja na kutoa mafunzo kwa ajili ya kuzuia ndoa za utotoni, ulinzi wa mtoto na mazingira wezeshi ya kwenda shule.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya ulinzi wa jamii, wafadhili wakubwa ni USAID, UNHCR, UNICEF, PLAN INTERNATIONAL na NORAD.

### 4.2.4 Uhifadhi wa Mazingira

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni washiriki muhimu katika ulinzi, uhifadhi na utunzaji wa Mazingira. Mashirika yalitekeleza shughuli zao kulingana na programu za Mazingira katika ngazi za Taifa, Mikoa, Wilaya na Ngazi ya Jamii.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya Mazingira imetumia kiasi cha Shilingi **52,324,452,813** sawa na asilimia **6** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya Utunzaji wa Mazingira kwa kupanda miti, kujenga uwezo katika kilimo hai, ulinzi wa maliasili, uhifadhi wa misitu, uhifadhi wa bahari pamoja na uhifadhi na ulinzi wa wanyama pori.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya Mazingira wafadhili wakubwa ni Jane Goodall Institute Canada/Australia/USA/Netherlands, USAID, WWF Germany, FORVAC, SIDA/EU na Nature Conservancy-HQ.

### 4.2.5 Sekta ya Kilimo

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametekeleza miradi ya kilimo hususani mafunzo na na kukuza uelewa wa wakulima wadogo, uongezaji wa thamani wa bidhaa, masoko, usambaji wa pembejeo za kilimo, ufugaji na huduma za ugani.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya Kilimo imetumia kiasi cha Shilingi 47,306,774,582 sawa na asilimia **5** ya fedha zote zilizotekeleza miradi.

Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya Kuwezesha na kuwajengea wakulima na maafisa ugani uwezo wa uzalishaji wa mazao bora na mbegu za kilimo, kukabiliana na tabia nchi pamoja na hali ya hewa katika mazingira husika.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya mazingira wafadhili wakubwa ni NORAD, AGRA, VI Agro Forestry, USAID, Bread for the World, Bill and Melinda Gates Foundation na Helvetas.

### 4.2.6 Sekta ya Elimu

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametekeleza miradi ya Elimu hususani ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu, ugawaji wa samani, vitabu na mahitaji mengine ya elimu.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya Elimu imetumia kiasi cha Shilingi **44,000,586,605** sawa na asilimia **5** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya mafunzo ya walimu ya namna ya kuboresha mbinu za ufundishaji, kuwajengea uwezo wazazi na walimu juu ya makuzi na malezi ya watoto katika ujuzi, ujenzi wa miundombinu ya shule, uendeshaji wa shule na kusomesha watoto yatima.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya elimu, wafadhili wakubwa ni Help to Help, Child Fund Korea, Irish AID, UK AID, German Fideral Ministry for Economic Cooperation and Development, PESTALOZZI Children Foundation, Feed the Children, We World Online Itally, HELVETAS, Segal Family Foundation, UNICEF, SDC na KOICA.

#### 4.2.7 Utawala Bora

Kwa mujibu wa mpango kazi wa Taifa wa Utawala Bora, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana mchango mkubwa katika kushawishi mabadiliko ya Sera na utekelezaji wa programu na mikakati ya kukuza utawala bora. Mashirika hayo yalitekeleza shughuli za elimu ya uraia pamoja na kuhimiza masuala ya Sheria, haki za binadamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

Kwa mwaka 2021, sekta ya utawala bora imetumia kiasi cha Shilingi **18,426,362,089** sawa na asilimia **2** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya mafunzo kuhusu elimu ya uraia, sheria, haki za binadamu na utawala bora, ushawishi na utetezi.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya Utawala Bora, wafadhili wakubwa ni DANIDA, USAID, EU,Embassy of Sweden na Norway.

#### 4.2.8 Sekta ya Maji

Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji (2002), mpango wa maendeleo na usimamizi wa usambazaji wa maji vijijini unahitaji mahusiano ya kitaasisi kati ya wadau muhimu ambao ni Serikali, Sekta binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii husika.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamehusika katika kutoa mchango kwa jamii katika upangaji, ubunifu, ujenzi na usambazaji wa vifaa, bidhaa na vipuri vinasohusiana na miradi ya maji nchini hususani maeneo ya vijijini.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya Maji imetumia kiasi cha Shilingi **10,449,181,801** sawa na asilimia **1** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji,uboreshaji wa huduma za maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na kwenye jamii.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya maji, wafadhili wakubwa ni WorldServe International, Play smaktir Hayat derrigi, UNICEF, Life water International, Stictching SMAVI na RALEIGH.

### 4.2.9 Haki za Binadamu

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalichangia katika kuendeleza na kuimarisha mfumo wa haki za binadamu nchini. Hii inahusisha ulinzi wa haki za binadamu, mahitaji ya makundi mbalimbali kama vile wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee na watu wenye maambukizi ya UKIMWI.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya haki za binadamu imetumia kiasi cha Shilingi **9,799,297,602** sawa na asilimia **1** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya kulinda na kutetea haki za wanawake na watoto, kuwajengea uwezo watetezi wa haki za binadamu kuhusu Sera na Sheria, kujenga uwezo wa kiuchumi kwa makundi mbalimbali,kutoa mafunzo juu ya haki za binadamu kwa wanasheria wa haki za binadamu,kutoa elimu ya Sheria na huduma ya msaada wa kisheria.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya haki za binadamu, wafadhili wakubwa ni SIDA, European union, We World Onlus Foundation (ITALY).

### 4.2.10 Usawa wa Kijinsia

Kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Usawa wa Kijinsia (2002) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kukuza uelewa wa jamii kupitia uhamasishaji, utoaji elimu

na kuijengea uwezo jamii, utoaji wa huduma za kijamii na  uzingatiaji wa masuala ya jinsia na mafunzo.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya jinsia imetumia kiasi cha Shilingi **4,517,067,410** sawa na asilimia 0.**48** ya fedha zote zilizotekeleza miradi. Uchambuzi unaonesha fedha nyingi za miradi zimeelekezwa katika masuala ya kuhamasisha wanawake kufahamu  haki kuhusu umiliki ardhi na kushiriki katika shughuli za maendeleo, kuimalisha usawa wa kijinsia na haki za wanawake,kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, uwezeshaji wanawake kiuchumi na kiuongozi.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya Jinsia, wafadhili wakubwa ni, Government of Canada-global affairs, BMZ-Germany na SIDA, USAID.  HELP AGE GERMANY.

### 4.2.11 Sekta ya Nishati

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamehusika katika uwezeshaji wa jamii katika masuala ya nishati ikijumuisha matumizi sahihi ya nishati, usambazaji wa umeme unaotumia nishati mbadala vijijini, namna bora ya kutumia nishati zilizopo katika shughuli za maendeleo kama vile kilimo kwa kutumia nishati ya jua na kutunza mazingira.

Kwa mwaka 2021, Sekta ya Nishati imetumia kiasi cha Shilingi 1,442,182,847 sawa na asilimia 0.15 ya fedha zote zilizotekeleza miradi.

Uchambuzi unaonesha kuwa katika sekta ya maji, wafadhili wakubwa ni Royal Norwegian Embassy, GIZ, WWF, SIDA, DFID-UK, MOTT Foundation na ENERGIA.


### 4.3 Wanufaika wa Miradi

Miradi iliyotekelezwa katika mwaka 2021 imenufaisha makundi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Jedwali hapa chini.

## Jedwali 4.3: Wanufaika wa Miradi kwa Kila Sekta/Afua

| SN | SEKTA | WANAWAKE | WATOTO | WANAUME | WAZEE | WAJANE | VIJANA | WATU WENYE ULEMAVU | TAASISI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **Afya** | 49,705,260 | 51,244,800 | 251,111 | 1,505,056 | 0 | 17378885 | 4,190 | 4,970,526 |
| **2** | **Uwezeshaji wa jamii** | 1,582,136 | 314,786 | 431,711 | 115,142 | 796 | 8,481,387 | 3,080 | 414,784 |
| **3** | **Ulinzi wa jamii** | 379151 | 375053 | 295867 | 1192479 | 24339 | 73399 | 2502 | 755,094 |
| **4** | **Mazingira** | 963,302 | 418,791 | 623,069 | 586,277 | 0 | 500,995 | 65 | 9,604 |
| **5** | **Kilimo** | 964,278 | 3,453 | 1,106,027 | 1,268 | 82 | 94,983 | 57 | 4,639 |
| **6** | **Elimu** | 2,766,804 | 507,136 | 9,204 | 0 | 0 | 3,052,505 | 952 | 9,592 |
| **7** | **Utawala Bora** | 3,870,542 | 2,589 | 3,208,460 | 0 | 0 | 1,002,208 | 35 | 1,166 |
| **8** | **Maji** | 27,245 | 48,983 | 15,077 | 33,497 | 0 | 32 | 0 | 113,618 |
| **9** | **Haki za binadamu** | 1,408,782 | 32,066 | 146,559 | 0 | 0 | 12,116 | 69 | 37,922 |
| **10** | **Jinsia** | 403,703 | 86,176 | 38,887 | 5 | 0 | 65,981 | 0 | 23 |
| **11** | **Nishati** | 123,751 | 581 | 508 | 73 | 0 | 285 | 0 | 452 |
| | **JUMLA** | 62,194,954 | 53,034,414 | 6,126,480 | 78 | 25,217 | 30,662,776 | 69 | 6,317,420 |

**Umbo 4.3: Asilimia ya Wanufaika kwa Makundi**




Uchambuzi unaonesha kuwa, Wanawake ndio wanaoongoza kwa kunufaika na miradi ya Mashirika sawa na asilimia 39.27, wakifuatiwa na Watoto ambao ni asilimia 33.49. Wanawake na Watoto wameongoza kwa kuwa miradi mingi hususan ile ya afya na uwezeshaji wa jamii imewalenga wao. Kutokana na uchambuzi, kundi lenye wanufaika wachache ni la watu wenye ulemavu. Vilevile, jumla ya taasisi 6,317,420 zikiwemo vijiji, shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali zimenufaika.


### 4.4 Ajira za Mashirika

Kwa mwaka 2021 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 955 yametoa jumla ya ajira **14,121** kwa makundi mbalimbali ikiwa na waajiriwa **8,344** na wanaojitolea **5,777**. Katika ajira hizo, uchambuzi unaonesha kuwa, watanzania ni **8,222** na wageni ni **122.**

**Jedwali 4.4 Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa kwa Watanzania na Wageni**

| Na. | Kundi | Watanzania walioajiriwa | Wageni walioajiriwa | Watanzania wanaojitolea | Wageni wanaojitolea | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vijana | 4,520 | 31 | 4,106 | 55 | 8,712 |
| 2 | Watu wazima | 3,636 | 86 | 1,419 | 96 | 5,237 |
| 3 | Wazee | 66 | 5 | 81 | 20 | 172 |
| | Jumla | 8,222 | 122 | 5,606 | 171 | 14,121 |

**Umbo 4.4 Asilimia ya Waajiriwa na Wanaojitolea**




Uchambuzi unaonesha kuwa Mashirika 10 yanayoongoza kwa kutoa ajira nyingi ni MDH (1,808), VST (507), World Vision Tanzania( 458), CCBRT (373), MSPH Tanzania LLC (350), Marie Stopes (337), Amref (330), Tanzania Health Promotion Support (THPS) (248), Medicins Sans Frontieres (216), International Rescue Committee (194).

## 4.5 Michango ya Hifadhi ya Jamii

Kwa mwaka 2021 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **139** yamechangia kiasi cha shilingi **12,700,469,371** katika hifadhi ya jamii hususan kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Katika uchangiaji huo, Mashirika yaliyofanya vizuri ni MSPH Tanzania LLC, Pathfinder International, Population Services International, Baylor College of Medicine, Medical Teams International, The Nature Conservancy, BBC Media Action, Action Aid Tanzania, Femina Hip na Sustainable Agriculture Tanzania.

# SURA YA TANO
# HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni mdau mkubwa wa maendeleo nchini. Aidha, inatambua kuwa Mashirika yanafanya kazi kubwa ya kujenga uwezo kwa wananchi hasa katika kujitambua na kutambua haki na wajibu katika kujiletea maendeleo kiuchumi na kijamii. Pia, inatambua kuwa kazi kubwa ya Serikali ni kujenga mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuweza kufanya kazi vizuri, kwa kufuata Sheria na Taratibu zilizowekwa.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama mdau wa maendeleo wa taifa yameendelea kutoa mchango mkubwa ambao unaonekana kupitia ajira na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika sekta za Afya, kilimo, uwezeshaji wa jamii kiuchumi, Elimu, Mazingira, haki za binadamu, utawala bora na Jinsia.

## 5.2 Changamoto

Kutokana na uchambuzi wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2021 changamoto zifuatazo zilijitokeza:-

a) Baadhi ya Mashirika kutowasilisha taarifa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Taarifa hizo zinajumuisha taarifa za robo mwaka, taarifa za mwaka na taarifa za mikataba au makubaliano ya fedha za wafadhili. Kutowasilisha taarifa hizo kunasababisha kutotambulika kwa mchango wa Mashirika hayo katika maendeleo ya jamii.
b) (kama taarifa zipo tujue ni mangapi yamebainika) Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushindwa kutumia mfumo wa kielektroniki (nis.jami.go.tz) kwa usahihi na hivyo kuwasilisha taarifa ambazo hazijakamilika hali ambayo inapelekea kushindwa kutambua mchango halisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa usahihi.

## 5.3 Mapendekezo

Katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya Mashirika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inatarajia kufanya yafuatayo:-

a) Kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Mashirika hayo na kutoa elimu juu ya Sheria, Taratibu na miongozo inayosimamia Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.
b) Kujengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau mbalimbali namna bora ya kuutumia mfumo wa kielektroniki (nis.jami.go.tz) ili kuweza kupata taarifa sahihi na kutambua mchango wa Mashirika hayo kwenye jamii.

## REJEA


JMT 1996. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jamii, 1996. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 1999. Mkakati wa Kitaifa wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Kitengo cha Uratibu.

JMT 2001. Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, 2001.

JMT 2002. Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.2002.

JMT 2002. Sera ya Taifa ya Usawa wa Jinsia na maendeleo ya Wanawake, 2002. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 2013. Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, 2013-2017, Wizara ya Katiba na Sheria.

JMT 2004. Kanuni ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Tangazo la Serikali 152, 2004.

JMT 2020. Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, 2020.

JMT 1977. Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1977.